MPANGO MKAKATI 2009 – 2013

THE FOUNDATION
for Civil Society

Shukurani

Kwa asasi yoyote inayojiendesha vyema, uandaaji wa dira kimkakati ni hatua muhimu ambayo lazima iitekeleze. Hii ni shughuli muhimu mno ambayo itaiwezesha asasi kujua ni wapi inakoelekea, jinsi itakavyofika huko inakotaka kwenda, lini na kwa njia zipi.

Mpango Mkakati wa Foundation, 2009 – 2013, unaanza rasmi katika nusu ya muongo wa pili, ambapo imekuwa ikisaidia ukuaji wa sekta ya Asasi za Kiraia nchini Tanzania. Ukichukulia maanani kwamba Foundation inafanya kazi katika njia chanya na pana zinazoshirikisha wadau kutoka nyanja mbalimbali, mchakato mzima wa kuandaa mpango mkakati ulikuwa ni wa ushirikishwaji wa hali ya juu, majadiliano, uchambuzi na hatimaye makubaliano katika maeneo muhimu ya matokeo kwa misingi ya vipaumbele vilivyoainishwa na ambavyo vinaakisi mahitaji ya walengwa, pia na mabadiliko tunayotarajia kuyaona yakitokea katika jamii.

Toleo hili la mpango mkakati linalolenga wadau wengi, lilitayarishwa kwa kutilia maanani ukweli kwamba maadili ya msingi na maelewano ya pamoja miongoni mwa wabia na wadau ni jambo muhimu sana ili mpango wowote ule uweze kufanikiwa. Mpango mkakati mpya wa miaka mitano (2009 - 2013) ni waraka wa kina ambao sio tu unaweka msisitizo katika zile programu za msingi ambazo Foundation inataka kuzifanikisha, lakini pia unajumuisha kwa upana wake mahitaji ya sekta ya asasi za kiraia katika kuitikia mahitaji na vipaumbele vya jamii vinavyoendelea kubadilika. Kwa sasa mkakati huu uko tayari, juhudi zimefanyika kuhakikisha unaeleweka kwa watu wengi zaidi, iwe rahisi kuutumia, ili watu wengi waweze kuusoma kwa urahisi, kuuelewa na kutafakari maudhui na maana yake.

Ni kwa misingi hii ndipo Foundation for Civil Society imefanya jitihada ya kuufanya Mpango mkakati wake wa mwaka 2009 – 2013 ufahamike kwa wadau wote. Hivyo basi, ni matarajio yetu kwamba wadau wote wataweza kusoma toleo hili la mpango mkakati lililo katika lugha rahisi, na hatimaye kutimiza wajibu wao muhimu katika utekelezaji wake.

Kwa misingi hiyo basi, The Foundation for Civil Society inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika mchakato mzima wa kuandaa mpango mkakati na utayarishaji wa toleo hili linalolenga wadau wote. Tunapenda kutoa ahsante zetu nyingi kwa asasi ya Hakikazi Catalyst ambao kutokana na utaalamu wao waliwezesha toleo hili kuyatarishwa.

Kupitia utekelezaji wa mpango mkakati huu, tunatarajia kuwa na Foundation iliyo imara na inayojituma zaidi ambayo inachangia kwa kiwango kikubwa katika kukua kwa sekta ya asasi za kiraia na kuwezeshwa kwa wananchi nchini Tanzania.

Dkt. Stigmata Tenga
Rais
The Foundation for Civil Society

Prudence Kaijage
Mwenyekiti wa Bodi
The Foundation for Civil Society

John Ulanga
Mkurugenzi Mtendaji
The Foundation for Civil Society

THE FOUNDATION
for Civil Society

Yaliyomo

Shukrani: i

1. **Ijue The Foundation for Civil Society:** 1

2. **Uongozi wa The Foundation for Civil Society:** 2

3. **Eneo Letu la Kazi: Hali Halisi ya Tanzania:** 3

4. **Hali ya Asasi za Kiraia Nchini Tanzania:** 4
   - Kuongezeka kwa umuhimu wa Asasi za Kiraia
   - Baadhi ya maoni kuhusu Asasi za Kiraia
   - Jukumu la The Foundation for Civil Society

5. **Mafanikio Yaliyokwisha Kupatikana na Mambo Tuliyojifunza** 6

6. **Lengo na Maudhui ya Programu:** 7
   - Lengo

7. **Ni Matokeo Gani Tunayotarajia?** 8
   - Eneo la Matokeo Muhimu la 1 – Sera
   - Eneo la Matokeo Muhimu la 2 – Utawala na Uwajibikaji
   - Eneo la Matokeo Muhimu la 3 – Kuimarisha Uwezo wa Asasi za Kiraia
   - Eneo la Matokeo Muhimu la 4 – Uwezo wa The Foundation for Civil Society

8. **Tutatekelezaje Programu Yetu?** 13
   - Makundi na maeneo lengwa
   - Huduma zetu
   - Ufuatiliaji na Tathmini
   - Fedha

9. **Mtazamo wetu kuelekea Maendeleo:** 16

THE FOUNDATION
for Civil Society

1. Ijue The Foundation for Civil Society

The Foundation for Civil Society ni Asasi ya Kitanzania inayowezesha watanzania pamoja na Asasi za Kiraia zinazojishughulisha na harakati za upunguzaji wa umaskini. The Foundation for Civil Society ilianzishwa mwaka 2003 na hivi sasa imekuwa mojawapo ya vyanzo vikuu vya uwezeshaji kifedha na mafunzo kwa Asasi za Kiraia za kitanzania.

Lengo letu ni kushirikiana na serikali na wananchi wote kwa ujumla katika kuhakikisha kuwa tunaishi katika Tanzania yenye amani tele, inayoongozwa vizuri na kidemokrasia, ambamo raia wake wanakuwa na kiwango cha juu cha elimu na wenye kuweza kujipatia maisha bora na endelevu katika uchumi imara na wenye kujali haki na usawa.

Lengo hili litafikiwa iwapo tu watanzania watafahamu haki na majukumu ya kila mmoja na jamii na wakiweza kudai uwajibikaji wa viongozi wao ili watekeleze majukumu kwa kuzingatia matakwa ya umma. Wakiwa na ufahamu mkubwa zaidi wa haki na wajibu wao, wananchi na jamii katika ujumla wake wanaweza kushirikiana kuleta mabadiliko yatakayo boresha maisha yao.

Kwa uwezeshaji wetu Asasi za Kiraia zitakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kushiriki katika maamuzi ya serikali na kuhakikisha kwamba sera kama vile MKUKUTA zinatekelezwa vizuri. Pia tunaiwezesha kuhakikisha kwamba serikali za mitaa zinatumia vizuri raslimali na kutoa huduma bora za jamii. Mwisho, The Foundation for Civil Society inaziwezesha Asasi za Kiraia kuhakikisha kwamba Bunge, Wizara, Wabia wa Maendeleo na sekta binafsi zinashirikiana vizuri kwa maslahi ya ustawi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Lengo letu
'Tanzania inafikia shabaha ya dira yake ya 2025 ya kukuza uchumi, kupunguza umaskini, kuimarika kwa utawala bora, na maisha bora kwa watanzania wote.'

Dira yetu
'Watanzania wenye kuwezeshwa kutambua haki zao na wenye kujishirikisha katika mchakato wa kujiletea mabadiliko yanayoboresha kiwango cha ubora wa maisha yao.'

Dhamira yetu
'Kuwawezesha wananchi kupitia utoaji wa ruzuku, kuwezesha mahusiano/ushirikiano na kusaidia kujenga utamaduni wa kupenda kujifunza miongoni wa Asasi za Kiraia'

Maadili yetu
'Haki, uadilifu, Kuzingatia utaalamu, uwazi, uwajibikaji na kuzingatia usawa na haki za kijinsia.

Foundation imejiwekea misingi ya maadili ili kusimamia utendaji kazi wake. Maadili haya ni haki, uadilifu, kuzingatia utalaamu, uwazi, uwajibikaji, na kuzingatia usawa na haki za kijinsia. Tunatumaini maadili haya yatakuwa ndiyo desturi kwa wabia wetu.

2. Uongozi wa The Foundation for Civil Society

The Foundation inaendeshwa na watanzania. Wabia wa maendeleo hutoa ushauri katika mipango na uwajibikaji na kuhakikisha kuwa tunaweza kupata fedha. The Foundation inaongozwa na Wanachama, Bodi ya Wakurugenzi na Sekretarieti. Majukumu ya kila kundi la uongozi yanaelezwa kwenye masanduku yafuatayo hapa chini:

Wanachama

Hawa ni wajumbe wasiopungua watano ama kuzidi saba, ambao huchaguliwa kutokana na kujitoa kwao katika kuboresha maisha ya jamii ya kitanzania. Hawa ndio wenye mamlaka ya juu kabisa katika The Foundation for Civil Society na wanawajibika kuteua wajumbe wa bodi ya wakurugenzi na wakaguzi wa mahesabu, sambamba na kuidhinisha mipango ya muda mrefu ya Foundation. Wanachama hutekeleza majukumu yao zaidi kupitia Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Foundation.

Bodi ya Wakurugenzi

Hali kadhalika Bodi ina wanachama kati ya watano na saba, ambao wajibu wao ni kutoa miongozo ya mara kwa mara katika utendaji wa Foundation. Bodi ya Wakurugenzi humteua Mkurugenzi Mtendaji wa shirika na kuidhinisha mabadiliko ya kanuni, taarifa za fedha na mipango ya Foundation kabla ya kuipeleka kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Sekretarieti

Sekretarieti inaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji na wajibu wake mkubwa ni utekelezaji wa kazi za Foundation. Mkurugenzi Mtendaji anawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi na hudumisha mahusiano na Wabia wa Maendeleo.

3. Eneo Letu la Kazi: Hali Halisi ya Tanzania

Katika sehemu hii tunaangalia takwimu zinazoelezea hali halisi ya Tanzania kuhusiana na masuala ya idadi ya watu, siasa, vyombo vya habari, uchumi, utawala, uwajibikaji na haki za binadamu.

Tanzania: Uhalisia na takwimu

Idadi ya watu	• Idadi ya watu ni milioni 42 kwa ukuaji wa ongezeko la takribani watu 1.2 kila mwaka • Karibu nusu ya watanzania wote wana umri ulio chini ya miaka 15 • Umri wa wastani wa kuishi kwa wanaume ni miaka 50, wakati wanawake ni miaka 53
Siasa na vyombo vya habari	• Tanzania ni nchi ya mfumo wa vyama vingi tangu mwaka 1992 • Jumla ya vyama vya siasa 18 vimepata usajili wa kudumu huku vinne tu vikiwa na uwakilishi Bungeni. • Chama cha Mapinduzi CCM kina asilimia 80 ya viti vyote Bungeni • Bunge limeanza kuonyesha uwezo mkubwa zaidi wa kuiwajibisha serikali • Utendaji wa Magazeti, radio na TV umekua sana katika miaka kumi iliyopita, hususani jijini Dar es salaam. • Vyombo vya habari vimezidi kuwa na nguvu katika kuiwajibisha serikali hata hivyo bado vinakabiliwa na vitisho pale vinapothubutu kuzungumzia masuala ya rushwa. • Kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya mtandao wa kompyuta (intaneti) japo bado ni ya kiwango cha chini • Matumizi ya simu za mkononi yamekuwa kwa kasi sana. Kati ya watanzania milioni 13 na 15 wana simu za mikononi.
Uchumi	• Sekta ya madini inaongoza kukua kwa kasi zaidi hata hivyo watu maskini hawaoni faida itokanayo na kukua huko • Kilimo huajiri asilimia 80 ya wafanyakazi na ndiyo sehemu kubwa zaidi ya uchumi wa nchi • Ukubwa wa kiwango cha umaskini maeneo ya vijini ni mara mbili zaidi ya maeneo ya mijini • Idadi ya watu wanaoishi kwenye umaskini inaongezeka • Tofauti kati ya watu maskini na matajiri inazidi kuongezeka.
Utawala na Uwajibikaji	• Rushwa ni tatizo kubwa katika utoaji huduma na katika mfumo wa sheria na haki nchini • Upatikanaji wa habari zinazohusu fedha ni mgumu sana katika ngazi za serikali za mitaa. Ni asilimia 15 tu ya vijiji ndivyo vyenye mbao za matangazo zenye kubeba taarifa mbalimbali kwa wakati. • Ni asilimia 25 tu ya watanzania ndiyo wanaojiona kuwa wenye ujasiri wa kuweza kuihoji serikali kuhusiana na taarifa za matumizi ya raslimali za umma.

Upatikanaji wa Haki za Binadamu, Huduma za Elimu na Afya	• Tanzania imetia sahihi makubaliano mengi ya kimataifa kuhusu haki za binadamu, hata hivyo inakabiliwa na changamoto ya kuzipitia upya baadhi ya sheria zake za kibaguzi zilizopitwa na wakati ili ziendane na makubaliano haya • Wanawake bado wameendelea kunyimwa haki zao kutokana na sheria za kimila zinazosimamia masuala ya mirathi sambamba na ukosefu wa huduma bora za wanawake wazazi • Zaidi ya watoto milioni moja wanatumikishwa kote nchini • Watu wachache tu ndiyo wanaoelewa haki zao za kisheria.Sheria nyingi zimeandikwa kwa Kiingereza, lugha ambayo watanzania wengi hawaielewi. • Theruthi mbili ya watanzania hawana uhakika wa kupata matibabu kutokana na kushindwa kumudu gharama. • Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watoto walioandikishwa shuleni, kumekuwepo upungufu mkubwa wa walimu wenye sifa • Watu wenye ulemavu wana fursa finyu ya kuzifikia huduma nyingi muhimu pamoja na ajira

4. Hali ya Asasi za Kiraia Nchini Tanzania

Kwa kiasi kikubwa kazi za Foundation hufanywa kupitia Asasi za Kiraia. Kwa hivyo ni muhimu tukaelewa jinsi sekta hii inavyokua, mtazamo wa wananchi kuhusu Asasi za Kiraia, na changamoto zinazozikabili Asasi zinazojishughulisha na upunguzaji wa umaskini. Katika sehemu hii tunayaangalia masuala haya ili kufafanua sababu yetu ya kusaidia sekta hii.

Kuongezeka kwa umuhimu wa Asasi za Kiraia

Miaka kumi iliyopita imeshuhudia kuongezeka kwa uelewa wa thamani ya Asasi za Kiraia miongoni mwa wananchi, na kwa kiasi kidogo hata serikali imezidi kutambua umuhimu huo. Hivi sasa Asasi za Kiraia (AZAKi) zimekubalika kama wadau katika maendeleo na katika utekelezaji wa sera na mipango ya serikali kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).Hali kadhalika AZAKi zimekuwa mstari wa mbele zikijishirikisha katika mpango mpya wa kuhakikisha kunakuwepo mawasiliano mazuri kati ya serikali, wafadhili na wananchi. Baadhi ya Asasi za Kiraia zinafanyakazi na Bunge ili kuhakikisha kwamba sheria mpya, sera pamoja na bajeti zinakuwa na manufaa kwa watu maskini, watanzania walioko katika mazingira hatarishi na walioachwa pembezoni. Hata hivyo, bado inahitajika kazi kubwa kuhakikisha kuwa asasi za kiraia zinashiriki na kushawishi kwa ufanisi zaidi michakato ya sera za kitaifa.

Asasi nyingi kubwa na zenye uwezo zinazoshiriki katika mijadala ya sera zina makao makuu jijini Dar es Salaam. Kati ya Asasi za Kiraia 3200 nchini, Asasi 600 ziko jijini Dar es Salaam. Hii inamaanisha kwamba maeneo ya vijijini yanakosa fursa za sauti zao kusikika katika ngazi ya taifa ya serikali. Kuna umuhimu mkubwa wa kuwezesha ujengaji uwezo wa asasi za vijijini.

Wahisani wanabadili namna ya kuwezesha maendeleo nchini Tanzania. Fedha nyingi zaidi kutoka mataifa wahisani zitachangia bajeti ya serikali badala ya kwenda moja kwa moja kwenye miradi mbali mbali. Kwa kuwa sasa wahisani watatumia muda mwingi jijini Dar es Salaam, ni muhimu Asasi za

Kiraia zikahakikisha kuwa malengo ya maendeleo yaliyowekwa yanafikiwa, kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji na bajeti, hususan kwenye maeneo ya vijijini.

Baadhi ya maoni kuhusu Asasi za Kiraia

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Foundation, wana jamii wengi wanathamini mchango wa Asasi za Kiraia. Watu wanne kati ya watano walisema kwamba wanadhani Asasi za Kiraia zinaleta manufaa katika jamii kwa kuwezesha kupunguza umaskini na kwa kupigania haki za watanzania wanyonge zaidi. Hata hivyo baadhi ya watu walizikosoa Asasi za Kiraia kwa madai kwamba zinalenga kujitajirisha zenyewe kuliko kusaidia kuinua hali ya maisha ya jamii, na kwamba baadhi zimekithiri kwa rushwa na mara nyingi hazishirikishi jamii katika upangaji mipango.

Wafanyabiashara pia walikuwa na mtazamo chanya kwa Asasi za Kiraia. Karibu watu wote walioshiriki utafiti huo walieleza kuwepo kwa umuhimu mkubwa wa sekta ya biashara na Asasi za Kiraia kushirikiana kwa karibu zaidi. Hii inamaanisha kwamba kuna fursa kubwa ya Asasi za Kiraia kufanya kazi kwa karibu na sekta ya biashara katika kuhakikisha jamii inanufaika zaidi.

Kwa upande mwingine, mara nyingi serikali inadai kwamba Asasi za Kiraia zinakosoa sana sera za serikali. Serikali pia inadai kwamba Asasi za Kiraia zilizomstari wa mbele kuikosoa serikali kwa kukithiri kwa rushwa nazo pia zinanuka rushwa.

Jukumu la The Foundation for Civil Society

Nafasi ya wananchi pamoja na Asasi zao za Kiraia ni muhimu sana katika kupunguza umaskini na kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla. Utawala na uwajibikaji utaimarika na kuwa bora zaidi pale tu kila mtanzania atakapokuwa na uwezo wa kuuhimiza. Sera zinaweza kufanikiwa pale tu wananchi wanapohisi kuwa zipo kwa ajili ya maslahi yao na wanapohimizwa kuhakikisha kuzitekeleza.

Jukumu la The Foundation for Civil Society ni kuwawezesha watanzania kujua haki zao na kuweza kujiletea mabadiliko. Tunaweza kuwawezesha wananchi kupitia Asasi zao za Kiraia kwa namna kuu tatu; kwa kutoa ruzuku, kwa kutoa mafunzo na kwa kuimarisha ushirikiano na mahusiano baina ya Asasi zenye malengo yanayoshabihiana. Tunaona fursa kubwa zaidi hivi sasa ambapo serikali imezidi kuonyesha nia njema na pia, kuwepo kwa ushirikiano mzuri zaidi kakti ya asasi za kiraia na vyombo vya habari, wabia wa maendeleo na sekta binafsi.

5. Mafanikio Yaliyokwisha Kupatikana na Mambo Tuliyojifunza

Foundation imefanikiwa katika mambo mengi tangu ilipoanzishwa mwaka 2003. Baadhi ya mafanikio haya yameorodheshwa kwenye kisanduku upande wa kulia. Takribani miradi 1,400 ya asasi za kiraia imepokea ruzuku na karibu theluthi ya Asasi zote za Kiraia nchini Tanzania zimepatiwa mafunzo ya matumizi na usimamizi wa ruzuku. Vile vile tumerahisisha mchakato wa maombi ya ruzuku ili kuwezesha Asasi changa za Kiraia kuomba ruzuku. Nyingi ya Asasi za Kiraia tulizofanya nazo kazi zimeripoti kwamba uwezo wake wa kiutendaji na usimamizi wa miradi umeboreka zaidi.

Sambamba na mafanikio haya yapo mambo mengi tuliyojifunza. Mambo tuliyojifunza yametusukuma kubadili namna tunavyotarajia kufanya kazi. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ambayo matunda yake yataboresha maisha ya wananchi. Hapa chini tunayataja mabadiliko makubwa matatu:

Mafanikio tangu mwaka 2003

- Kuboreka kwa ufahamu wa wananchi juu ya sera za serikali na haki katika jamii
- Dola za kimarekani milioni 16 zimetolewa kama ruzuku kwa Asasi za Kiraia 1,380
- Zaidi ya asasi 1,000 zimepatiwa mafunzo ya usimamizi wa ruzuku
- Asasi za Kiraia zipatazo 300 zimepatiwa mafunzo ya uongozi wa Asasi, utafutaji raslimali fedha, ufuatiliaji na tathmini, ubia na uchambuzi wa sera.
- Midahalo 46 kuhusu utawala bora na upunguzaji umaskini imefanyika nchi nzima
- Tovuti 50 za Asasi za Kiraia zimetengenezwa
- Kukua kwa ushirikiano na Bunge

Tutafanya kazi zaidi maeneo ya vijijini

Licha ya huduma zetu kuhitaji nchi nzima, tutaelekeza nguvu kubwa kwenye maeneo ya vijijini yenye kupata huduma chache zaidi. Katika mpango mkakati huu tutatenga asilimia 70 ya ruzuku na mafunzo kwa Asasi zilizoko maeneo ya vijijini, au kwa Asasi za Kiraia zilizoko mjini lakini zinazofanya kazi kubwa vijijini.

Tutahakikisha kuwa mafunzo na ruzuku tunazotoa zinazaa matunda

Huko nyuma tulielekeza nguvu kubwa katika kuzipatia Asasi za Kiraia ruzuku na mafunzo ili kuboresha uwezo wa kutekeleza majukumu. Tumetumia muda kidogo sana katika kuangalia matokeo ya kazi zinazofanywa na Asasi husika. Katika kipindi hiki hadi ifikapo mwaka 2013, tutaelekeza raslimali zaidi kwa Asasi za Kiraia zitakazoweza kuonyesha kuwa zinawawezesha wananchi kuwawajibisha viongozi wao na zenye kuchangia kuleta mabadiliko katika sera za serikali pamoja na shughuli zenye kuwanufaisha wananchi maskini na watu walioko katika mazingira hatarishi.

Tutajibidisha kuhakikisha Foundation inakuwa na uwezo zaidi na kuwa yenye uhakika kifedha

Hadi sasa Foundation imekuwa ikipokea fedha kutoka kwa wafadhili kutoka mataifa ya nje ya Tanzania. Hili ni tatizo katika upangaji wa mipango ya muda mrefu kwani wakati mwingine wafadhili huweza kubadili vipaumbele juu ya maeneo wanayotaka kuelekeza fedha zao. Inaweza kuwa vigumu kwetu kupanga mipango ya muda mrefu tunapokuwa hatuna uhakika wa kiasi cha fedha tutakachoweza kupata. Siku zijazo tutajaribu kutafuta fedha kutoka wigo mpana zaidi wa makundi ya wahisani ili tuweze kuhakikisha kuwa tunakuwa na fedha za kutosha kuongeza na kuboresha kazi za Foundation.

6. Lengo na Maudhui ya Programu

Sehemu hii inaiangalia mipango yetu hadi mwaka 2013. Kwanza, tunazungumzia jinsi ambavyo kazi za Foundation zitafikia lengo lake. Kisha tunayaangalia maeneo matatu muhimu ya kimaudhui yanayohusika.

Lengo

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inaitazama Tanzania kuwa nchi yenye amani tele, yenye kuongozwa vizuri kidemokrasia, ambamo raia wake wanakuwa na kiwango cha juu cha elimu na wenye kuweza kujipatia maisha bora na endelevu katika uchumi imara na wenye kujali haki na usawa.

Maeneo muhimu (maudhui) ya Programu

Ili kufikia malengo, Foundation itaziwezesha Asasi za Kiraia zinazofanya kazi ili kuleta mabadiliko katika maeneo matatu muhimu yafuatayo:

> 'Kujenga msingi unaowawezesha wananchi kuwa nguvu kubwa na muhimu ya kuleta mabadiliko katika kuboresha utawala wa kidemokrasia nchini Tanzania, katika kupambana na umaskini na katika kuhakikisha wanafikia maisha bora kwa kila mtanzania.'

Sera – Sera za serikali zina matokeo ya moja kwa moja katika maisha ya kila siku ya watanzania wote. Kwa hiyo ni muhimu kuhakikisha kwamba wananchi wote wanashiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi kuhusiana na sera na katika kuhakikisha kuwa sera hizo zinatekelezwa kikamilifu na kwa usahihi.

Utawala na uwajibikaji – Ngazi zote za serikali zinawajibika katika kuhakikisha kuwa zinatumia vizuri na kwa usahihi raslimali za umma (ikiwemo fedha) pamoja na kutoa vizuri huduma za jamii. Wananchi hawana budi kuhimiza na kudai serikali, hususan serikali za mitaa, kufanya kazi zake vizuri, kwa haki na kwa uwazi.

Michakato ya kisiasa – ili kuhakikisha kuwa malengo ya maendeleo ya taifa yanafikiwa hapana budi makundi mbali mbali ya watu kushirikiana. Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba Rais, Wizara, Bunge, Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo wanafanya kazi kwa namna ambayo itawanufaisha wananchi wote kwa usawa.

7. Ni Matokeo Gani Tunayotarajia?

Foundation imeamua kufanikisha malengo yake katika maeneo manne muhimu, yanayoitwa, Maeneo ya Matokeo Muhimu: Ushiriki katika Sera, Utawala na Uwajibikaji, Kuimarisha uwezo wa Asasi za Kiraia na uwezo wa Foundation. Kila moja ya maeneo haya ya matokeo muhimu lina lengo kuu. Ili kufahamu iwapo tunafikia shabaha ya lengo kuu, tumebuni malengo mahsusi chini yake, ambayo tumeyaita viashiria vya utendaji, ambavyo vinaweza kupimika. Hapa chini tunaangalia kwa undani zaidi malengo hayo, shughuli na viashiria kwa kila eneo la matokeo muhimu.

Eneo la Matokeo Muhimu la 1 – Sera

Lengo: Wananchi wanashiriki kushawishi na kufuatilia michakato ya sera ili kuboresha utoaji wa huduma.

Ni shughuli zipi tutakazowezesha?

Foundation itaziwezesha Asasi za Kiraia kuwaelimisha wananchi juu ya sera mbali mbali zinazogusa maisha yao na zile zinazowawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi ya nini kinapaswa kuwemo kwenye sera. Pindi wananchi wanapoelewa jinsi sera ama sheria mpya zitakavyowaathiri, wanaweza kujipanga na kudai mabadiliko yatakayo linda na kuboresha maisha yao. Vile vile, wananchi wanapoelewa vizuri lengo la sera za serikali, wanaweza kuhakikisha kuwa sera hizo zinatekelezwa vizuri.

Ili kufanikisha lengo hili, tutaziwezesha Asasi za Kiraia kuwapatia wananchi na jamii machapisho yaliyoandikwa kwa lugha rahisi ya sera na sheria muhimu kwa maisha yao. Tutaelekeza nguvu kubwa ya kazi hii katika maeneo ya vijijini na yale yenye huduma chache au duni za kijamii na tutahakikisha kuwa sauti za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zinasikika.

Shughuli muhimu

- Kuongeza uelewa na ufahamu wa sera
- Kuunganisha nguvu za wananchi
- Kuwawezesha wananchi kujadiliana na serikali
- Kufanya tafiti zenye ubora ili kusaiidia kuipa taarifa serikali
- Kuyashirikisha makundi yaliyokatika hatari zaidi ya kuathirika
- Kuleta mabadiliko!

Tutaziunga mkono Asasi za Kiraia katika kuwawezesha wananchi kuunganisha nguvu, kuhimiza uwajibikaji na kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi kwenye ngazi zote za utawala; mikutano mikuu ya vijiji, kamati za maendeleo za kata, halmashauri za wilaya na katika ngazi ya tawala za mikoa. Asasi za Kiraia zinayo nafasi nzuri ya kuwezesha hoja na mitazamo ya wananchi kujulikana kupitia mikutano mbali mbali pamoja na matumizi ya vyombo vya habari.

Njia mojawapo nzuri na sahihi ya kuhakikisha kuwa mitazamo na hoja za wananchi zinafika ngazi ya kitaifa ni kwa kupitia taarifa za tafiti zenye ubora wa kiwango cha juu kufikishwa kwenye idara na wakala wa serikali. Ni dhahiri hivi sasa serikali katika ngazi ya taifa ina fursa finyu sana ya kupata taarifa juu ya kinachotendeka katika ngazi za chini yaani ngazi ya jamii. Mara nyingi sera na sheria hutungwa pasipokuwa na taarifa zote muhimu. Kwa hali hii, Asasi za Kiraia zinaweza kuziba pengo lililopo kati ya wananchi na serikali.

Ni viashiria vipi tunaviangalia?

Ifikapo mwaka 2013, tunataka tuwe na uwezo wa kusema kuwa:

- Asasi nyingi zaidi za kiraia zinafahamu na kuzielewa sera na sheria zinazogusa na kuathiri maisha ya wananchi.
- Watu wengi zaidi, ikiwa ni pamoja na wanawake na makundi mengine yaliyo katika hatari ya kuathirika, wanashiriki kikamilifu katika mijadala ya umma kuhusu sera na wanaweza kusema kuwa wamechangia kuleta mabadiliko.
- Watu wengi zaidi wanaridhishwa na utoaji wa huduma za umma.
- Zaidi ya nusu ya Asasi za Kiraia tunazoziwezesha zinashiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi ya sera na zinashawishi mabadiliko kufanyika.

Eneo la Matokeo Muhimu la 2 – Utawala na Uwajibikaji

Lengo: Wananchi wanakuwa na ufahamu wa haki na wajibu wao na wanaohimiza uwajibikaji katika usimamizi wa raslimali za umma.

Ni shughuli zipi tutakazowezesha?

Katika halmashauri za wilaya na manispaa nyingi, wananchi wengi pamoja na Asasi za Kiraia zinashindwa kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi kutokana na kutokuwepo kwa taarifa zinazoeleweka kuhusu mipango na bajeti za serikali zao za mitaa. Foundation itaziwezesha Asasi za Kiraia kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa jinsi serikali za mitaa zinavyoandaa mipango yake. Pia, tutajibidisha kuhakikisha kuwa haki za wananchi kupata taarifa sahihi na za wazi kuhusu bajeti, mipango na matumizi zinatambuliwa na kuheshimiwa. Asasi za Kiraia zinapokuwa na taarifa hizi pamoja na kuwa na uelewa mzuri, zinakuwa na uwezo mzuri zaidi wa kuwawezesha wananchi kushirikiana na watumishi wa serikali na viongozi wao katika kupanga vizuri matumiizi ya raslimali za umma.

Matumizi mabaya ya raslimali za umma yanachelewesha upunguzaji wa umaskini. Tutawezesha shughuli zinazoelekeza katika kuziwajibisha serikali juu ya matumizi ya fedha za

Shughuli muhimu

- Kuongeza ushiriki wa wananchi katika michakato ya mipango na bajeti ya serikali za mitaa
- Kuhimiza na kutimiza haki ya wananchi kupata taarifa/habari
- Kuwasaidia wananchi kufanya ufuatiliaji wa bajeti na huduma
- Kutumia vyombo vya habari kujadili masuala ya uwajibikaji
- Kuongeza ufahamu juu ya haki za wananchi
- Kuhimiza kuwepo kwa sekta binafsi inayotimiza wajibu
- Kuwaelimisha wapiga kura juu ya thamani ya haki yao ya kidemokrasia

umma na utoaji wa huduma za umma. Shughuli hizi zitajumuisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma, ambayo humaanisha kufuatilia fedha za umma kutoka wilayani hadi zinapowafikia wananchi ili kuhakikisha kuwa zinatumika vizuri kama ilivyokusudiwa au kupangiliwa. Hali kadhalika, tutawezesha tafiti zitakazojikita katika kutathmini ubora wa huduma za umma na kiwango cha rushwa. Pia tutazihimiza Asasi za Kiraia kutumia vyombo vya habari kama radio, TV na magazeti katika kutangaza masuala ya uwajibikaji. Kazi hizi zitasaidia kuhakikisha kwamba watumishi wa serikali wanatimiza wajibu wao ipasavyo.

Wananchi wengi hawafahamu haki zao; haki chini ya sheria za Tanzania, haki za kikatiba na haki za binadamu kwa ujumla. Baadhi ya mifano ya haki hizi ni pamoja na haki za umiliki na matumizi ya ardhi, haki za ajira na haki za usawa wa kijinsia. Tutawezesha shughuli zinazolenga kuwaelimisha wananchi kuhusu haki zao. Pia tutaunga mkono Asasi za Kiraia zinazoendesha kampeni dhidi ya sheria zinazowabagua wanawake pamoja na makundi mengine yaliyo katika hatari zaidi ya kuathirika kwa namna mbalimbali. Vile vile Asasi za Kiraia zitahimizwa kushirikiana na kampuni za biashara binafsi ili kuhakikisha kuwa zinaboresha na kuinua maisha ya watu maskini nchini Tanzania badala ya kuwanyonya na kuwadidimiza zaidi.

Mara nyingi sana, wananchi hutoa kura zao kirahisi kabisa kisha hawawaoni wabunge ama madiwani wao hadi uchaguzi mwingine unapowadia. Tutasadia programu zinazolenga kukuza na kueneza elimu ya wapiga kura ili kuhakikisha kwamba chaguzi zinakuwa za haki na kuwa viongozi wanaochaguliwa wanatimiza wajibu wao ipasavyo.

Ni viashiria vipi tunaviangalia?

Ifikapo mwaka 2013, tunataka tuwe na uwezo wa kusema kuwa:

- Watu wengi zaidi wanaomba na kupata taarifa na maelezo kuhusu utendaji wa serikali katika ngazi zote za mitaa na ngazi ya taifa.
- Idadi ya wanawake wanaochaguliwa katika ngazi ya udiwani imeongezeka mara tatu zaidi.
- Wananchi wengi zaidi wanapata taarifa kupitia mbao za matangazo na wanashiriki kikamilifu kwenye mikutano ya vijiji
- Wananchi wengi zaidi wanahimiza uwajibikaji katika matumizi ya raslimali za umma kwenye maeneo yao.
- Wananchi katika wilaya nyingi zaidi wanasaidiwa kupata haki zao kupitia wasaidizi wa kisheria '*paralegals*' waliopatiwa mafunzo
- Sheria kandamizi na za kibaguzi zinafanyiwa marekebisho
- Karibu watanzania wote wanashiriki katika chaguzi mbali mbali na wanahakikisha kuwa wabunge na madiwani wao wanawajibika ipasavyo.

Eneo la Matokeo Muhimu la 3 – Kuimarisha Uwezo wa Asasi za Kiraia

Lengo: Asasi za Kiraia zinakuwa na ubunifu, endelevu na zenye kuwajibika

Shughuli muhimu

Kutoa mafunzo kwa Asasi za Kiraia ili:-

- Kuboresha uongozi wa ndani ya Asasi
- Kuimarisha mipango na usimamizi wa fedha
- Kukataa rushwa na kuboresha uwajibikaji
- Kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano

Kutoa fursa kwa Asasi za Kiraia ili

- Kujenga mahusiano na Asasi nyingine za Kiraia
- Kukutana na wawakilishi wa wananchi
- Kupata ushauri kutoka The Foundation

Ni shughuli zipi tutakazowezesha?

Asasi za Kiraia zilizo imara ni muhimu sana katika kufikia lengo letu kuu. Asasi zenye kuzingatia taaluma na utalaamu zinazoheshimiwa na wananchi pamoja na serikali zinaweza kuleta mabadiliko katika maisha ya watanzania maskini na wale walioko katika hatari zaidi ya kuathirika. Tutaziwezesha Asasi za Kiraia kuwapatia mafunzo watumishi wake katika viwango vya juu, kupanga vizuri na kuzifanya kazi zao kuwa zenye ufanisi kwa watu na jamii zinamofanyakazi. Kipekee tutaziwezesha Asasi hizi katika masuala ya uongozi na masuala ya fedha. Mashirika yote tunayoyawezesha yatahimizwa kutumia kikamilifu teknolojia ya habari na mawasiliano katika kazi zao. Tutafanya bidii kuhakikisha kwamba Asasi za Kiraia tunazoziwezesha haziivumilii ama kuionea haya rushwa kwa namna yoyote. Tutazitembelea Asasi tunazoziwezesha ili kuhakikisha kuwa zinaendeshwa vizuri, zikitoa matokeo mazuri na kuona kwamba mahitaji yao ya mafunzo yanatoshelezwa. Pia, tutatoa fursa kwa Asasi tunazozisadia kukutana na Asasi nyingine za kitanzania na za kimataifa ili ziweze kubadilisha taarifa na uzoefu. Kila mwaka tutaandaa mkutano baina ya Asasi tunazoziwezesha na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania pamoja na wawakilishi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Foundation itatoa kipaumbele kwa mashirika makubwa yenye uongozi madhubuti yanayoweka msisitizo wa kipekee katika kufuata sheria zilizomo kwenye katiba zao. Hapa lengo la Foundation ni kwamba mashirika tunayoyawezesha hatimaye yataanza kujitegemea.

Ni viashiria vipi tunaviangalia?

Ifikapo mwaka 2013, tunataka kuona kwamba:

- Asasi za Kiraia tunazoziwezesha zinajipanga vizuri na kuwa na ufanisi
- Asasi nyingi zaidi za kiraia zinashiriki kikamilifu katika mijadala ya sera kwenye ngazi za wilaya na kitaifa
- Asilimia 80 ya Asasi za Kiraia zinaweka wazi kwa umma taarifa zao za fedha na za mwaka
- Asasi za Kiraia zinakuwa na mahusiano mazuri na Asasi nyingine, jamii zinamofanya kazi, viongozi waliochaguliwa na watumishi wa serikali

Eneo la Matokeo Muhimu la 4 – Uwezo wa The Foundation for Civil Society

Lengo: Foundation inakuwa na uwezo mkubwa wa kutoa huduma bora kwa ufanisi na utoshelevu

Tutafanya nini kufikia lengo hili?

Foundation ni moja ya watoaji wakubwa wa fedha kwa mashirika ya Kiraia nchini Tanzania. Ili tuweze kuboresha na kuendelea kutoa misaada kwa asasi za Kiraia hatuna budi kwanza kuhakikisha kuwa watumishi wa Foundation ni wenye sifa bora na wanazifikia kirahisi taarifa bora na sahihi zinazohitajika ili waweze kufanya maamuzi sahihi. Hali kadhalika hatuna budi kujihakikishia kuwa tunakuwa na vyanzo vya kuaminika vya fedha kwa kipindi cha muda mrefu.

Maamuzi yetu yote yatazingatia ushahidi utakaotokana na tafiti zenye ubora wa kiwango cha juu. Tutafanya tafiti za mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa misaada tunayoitoa kwa Asasi za Kiraia inakuwa na matokeo mazuri yaliyotarajiwa. Kila mwaka tutatangaza matokeo ya tafiti kuhusu ufanisi wa Asasi za Kiraia nchini Tanzania. Foundation itaendeleza maktaba ya kawaida na ile ya kwenye mtandao wa intaneti (maktaba tando) kwa matumizi ya wananchi.

Uendelevu wetu kifedha utaimarishwa na kuboreshwa kwa kupanua wigo wa vyanzo vyetu vya mapato, kitaifa na kimataifa. Tunatarajia kuongeza kipato chetu kwa kuyatoza ada mashirika mengine makubwa yatakayohitaji huduma zetu. Mwisho, tutaboresha mazingira yetu ya kazi ili tuweze kuwavutia na kuwafanya wakae kwa muda mrefu watumishi wenye sifa bora ili waweze kuendesha sekretarieti yetu kwa ufanisi zaidi.

Ni viashiria vipi tunaviangalia?

Tunataka kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2013:

- Foundation iwe ikipokea mapato yake zaidi kutoka kwenye sekta ya biashara, mashirika ya kimataifa na watu binafsi
- Maamuzi yetu yote kuhusu ruzuku, huduma na sera yatokane na taarifa za tafiti zenye ubora wa kiwango cha juu
- Foundation inakuwa mahali pazuri pa kuvutia kwa watumishi wenye sifa bora zaidi

Shughuli muhimu

- Kutumia taarifa zitokanazo na tafiti bora katika kufanya maamuzi
- Kutafuta vyanzo mbadala madhubuti vya mapato
- Kuboresha maktaba yetu ya kawaida na ile ya kwenye mtandao
- Kuboresha mazingira yetu ya kazi

8. Tutatekelezaje Programu Yetu?

Katika sehemu hii tunaangalia aina za mashirika tutakayofanya nayo kazi kisha tutatoa maelezo ya aina ya huduma tutakazotoa na kueleza namna tutakavyofanya ufuatiliaji wa kazi zetu.

Makundi na maeneo lengwa

Makundi muhimu zaidi kwa kazi za Foundation ni pamoja na watu maskini, watu walio katika hatari zaidi ya kuathirika na watanzania walioachwa pembezoni. Ifikapo mwaka 2013, tunakusudia kwamba huduma zetu zitakuwa zimewafikia watu zaidi ya milioni kumi (10). Kama tulivyokwisha kueleza hapo awali, walau asilimia 70 ya misaada yetu italenga maeneo ya vijijini. Vile vile tutaunda ubia na mashirika mengine, mitandao ya Asasi za Kiraia na watu binafsi ili kutimiza malengo yetu ya kuifikia kila wilaya nchini.

Hapa chini tumeorodhesha aina ya Asasi za Kiraia tutakazozipa huduma zetu:

- Asasi zisizo za Serikali
- Vyama vya kitaalamu
- Vyama vya Wafanyakazi
- Mashirika ya Kidini
- Jumuiya za Kijamii
- Ushirika
- Mashirika ya Habari
- Asasi nyinginezo za Kiraia zinazoshughulika na masuala ya umaskini na utawala

Utakuwa umegundua kwamba baadhi ya mashirika ya kibiashara yameingizwa kwenye orodha hii. Hata hivyo hakuna shirika litakaloruhusiwa kufaidika kutokana na misaada yetu. Tutawezesha shughuli zile tu zenye maslahi kwa umma. Vile vile, licha ya kwamba tunatoa huduma kwa mashirika ya kidini, hatuhusishi makanisa ama misikiti kama sehemu ya wabia wetu.

Huduma zetu

Tunatoa huduma za aina mbili: ruzuku na kujenga uwezo

Ruzuku

Katika kipindi hiki hadi kufikia mwaka 2013, ruzuku zetu zitatolewa kwa Asasi za Kiraia zenye uwezo wa kufikia lengo letu la jumla na malengo ya kila eneo la matokeo muhimu. Tutatoa aina nne za ruzuku: ruzuku ya usajili, ruzuku ndogo ya mzunguko, ruzuku ya kiwango cha kati, na ruzuku ya kimkakati. Tunakusudia kupitisha kati ya maombi 300 na 350 ya ruzuku kila mwaka na kutoa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 8.7. Madhumuni ya ruzuku hizi yameelezwa kwenye jedwali lifuatalo:

Ruzuku za The Foundation for Civil Society

Aina ya ruzuku	Madhumuni ya ruzuku	Kiwango cha juu kwa Asasi (TSh)	Idadi za maombi ya ruzuku yanayoidhinishwa kila mwaka
Ruzuku ya usajili	Kusaidia vikundi vidogo ili viweze kusajiliwa na kuweza kuwa na sifa za kupatiwa ruzuku na Foundation.	200,000 (mara moja tu)	50-70
Ruzuku ndogo za mzunguko	Kuyawezesha mashirika kujenga na kukuza uwezo wao katika mbinu za uendeshaji, kuinua viwango vya uwajibikaji na uwezo wa kutekeleza miradi.	7,500,000 (kwa kipindi cha hadi mwaka mmoja)	140-160
Ruzuku ya kiwango cha kati	Kuziwezesha Asasi za Kiraia zenye uzoefu wa awali ili ziweze kukua kwa kutekeleza miradi mikubwa na yenye ufanisi zaidi.	45,000,000 (kwa mwaka hadi muda wa miaka mitatu)	100-120
Ruzuku ya kimkakati	Kuziwezesha Asasi za Kiraia zenye uzoefu ili kufikia malengo yao pamoja na malengo ya the Foundation for Civil Society.	125,000,000 (kwa mwaka hadi muda wa miaka mitatu)	10-12

Kujenga uwezo

Katika kipindi cha uhai wa mpango mkakati huu tutaendelea kutoa huduma za kujenga uwezo wa Asasi za Kiraia kama vile:

Fursa za mafunzo – mafunzo yetu yataziwezesha Asasi za Kiraia kuboresha na kuimarisha uongozi na mbinu za usimamizi wa fedha, kuelewa sera na kupigania mabadiliko na kufuatilia maendeleo ya kazi zinazofanywa na asasi hizo. Pia, mafunzo yatatolewa kuimarisha na kuboresha mbinu za ufuatiliaji wa matumizi ya raslimali za umma pamoja na ufuatiliaji wa uwajibikaji wa kijamii. Tunatarajia kwamba tutaendesha walau programu kumi (10) za mafunzo kila mwaka zikijumuisha washiriki 25 kwa kila programu.

Kuzitembelea Asasi ili kuzipa ushauri – tutafanya ziara kila mwaka ili kuziwezesha Asasi na kufuatilia mafunzo tunayotoa pamoja na kutoa ushauri kuhusiana na utekelezaji wa programu mbali mbali.

Tathmini ya uwezo wa Asasi – tutafanya tathmini kila mwaka ili kuziwezesha Asasi kubainisha maeneo zinayopaswa kuboresha uwezo wake. Vile vile Asasi tano zitasaidiwa kuandaa mipango mkakati na miongozo ya Asasi hizo.

Huduma za kuimarisha uhusiano – tutaendelea kutoa fursa za mikutano na kubadilishana mawazo miongoni mwa Asasi za Kiraia na baina ya Asasi za Kiraia na wadau wengine kama vile Wabunge na Wawakilishi, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki pamoja na sekta binafsi. Hata hivyo, tunatarajia Asasi za Kiraia tunazoziwezesha zitajenga mahusiano na Asasi nyingine pasipo kungoja mkono wa Foundation katika kulitekeleza jambo hili.

Ufuatiliaji na Tathmini

The Foundation for Civil Society itafuatilia na kutathmini utendaji wake wa jumla na programu zake pamoja na utendaji wa Asasi za Kiraia inazoziwezesha. Kwa vile lengo letu kuu ni kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na uwezo wa kudai haki zao na kuboresha maisha yao hivyo basi shughuli muhimu za ufuatiliaji wetu zitalenga zaidi ngazi ya mwananchi. Tutafanya ufuatiliaji wa maendeleo ya utendaji kwa njia nne zifuatazo:

Ufuatiliaji wa mchakato	Aina hii ya ufuatiliaji itafanyika wakati wote kwa kuangalia utekelezaji wa mipango na bajeti ya kila mwaka ya Foundation. Taarifa itatolewa kwa Bodi kila baada ya miezi mitatu.
Ufuatiliaji wa matokeo ya kipindi kifupi	Kila baada ya miezi sita tutatoa taarifa za kazi zetu na kazi za wabia wetu. Taarifa hizi zitatolewa kupitia vijarida na kwenye tovuti yetu.
Tathmini ya matokeo ya kipindi cha kati	Kila mwaka tutashirikiana na wabia wetu kuangalia maendeleo ya utendaji wetu kuelekea katika kufikia malengo ya maeneo ya matokeo muhimu ya Foundation. Matokeo ya tahmini hii yatatusaidia kuboresha namna tunavyofanya kazi na yatajumuishwa kwenye ripoti zetu za mwaka na pia yatawekwa kwenye tovuti yetu.
Tathmini ya mabadiliko	Hii ndiyo tathmini muhimu zaidi kwani inaangalia jinsi tunavyochangia kubadili maisha ya wananchi na itatupa picha ya maendeleo yetu kuelekea kufikia lengo kuu letu. Tathimini mbili za namna hii zitafanyika, moja katikati ya kipindi cha utekelezaji wa mpango mkakati huu na nyingine itafanyika mwishoni kabisa, hapo mwaka 2013. Kazi zetu pamoja na zile za wabia wetu zitafanyiwa tathmini huru.

Vile vile katika ufuatiliaji na tathmini tutalenga katika ngazi nne ambazo ni ngazi ya mwananchi, sekta ya Asasi za Kiraia, wabia wetu miongoni mwa Asasi za Kiraia na katika ngazi ya Foundation. The Foundation for Civil Society itaandaa mpango utakaotuwezesha kufuatilia na kupima maendeleo katika maeneo ya matokeo muhimu.

Ngazi ya mwananchi	Kazi yetu muhimu ya ufuatiliaji itakuwa katika kupima maendeleo ya utekelezaji kuelekea kufikiwa kwa shabaha zinazolenga wananchi katika Maeneo ya Matokeo Muhimu ya 1 na ya 2. Kabla ya kufanya kazi hii, tutapima kwanza hali halisi ya sasa katika maeneo haya ili uweze kuona iwapo tutakuwa tumechangia kuleta mabadiliko hapo baadaye.
	Vile vile tutapima idadi ya wananchi wanaonufaishwa na shughuli zinazofanywa na Asasi za kiraia tunazoziwezesha. Hii itahusisha idadi ya wanachama wa mashirika hayo na pia idadi ya watu wanaohudhuria mafunzo na mikutano ya uelimishaji jamii.
Ngazi ya sekta ya Asasi za Kiraia	Tutapima ukuaji na maendeleo ya Asasi za Kiraia nchini Tanzania. Vile vile tutaangalia masuala ambayo Asasi za Kiraia zinajishughulisha nayo, tutaangalia viwango vya maadili na mienendo pamoja na nguvu ya ubia na ushirikiano wake na sekta za siasa, binafsi na wahisani.

Ngazi ya wabia wetu wa Asasi za Kiraia	Tutahakikisha kwamba Asasi za Kiraia tunazozisadia zitatupatia taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa shughuli zao pamoja na taarifa za matumizi ya fedha. Asasi hizo zitatembelewa walau mara moja kwa mwaka ili kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa kazi zao pamoja na kutoa ushauri kila itakapobidi. Tathmini huru ya mchango wa kazi za Asasi tunazoziwezesha kwa maendeleo ya jamii itafanyika katikati ya kipindi cha utekelezaji wa mpango mkakati huu.
Ngazi ya The Foundation for Civil Society	Tutaangalia mara kwa mara katika utendaji wa kazi zetu ili kuhakikisha kuwa tunafanya kazi kwa ufanisi na kwa kufuata kanuni na sheria tulizojiwekea. Tathmini huru zitafanyika mara kwa mara.

Fedha

Jumla ya makisio ya bajeti ya kutekeleza mpango mkakati huu ni dola za Marekani milioni 58. Asilimia 20 ya fedha hizi itatumika katika shughuli za uendeshaji wa Foundation. Asilimia 80 itatumika kutoa ruzuku na huduma nyingine. Jedwali lifuatalo linaeleza kwa ufupi kuhusu bajeti yetu hadi mwaka 2013

MATUMIZI ($)	2009	2010	2011	2012	2013	TOTAL	%age
Ruzuku na Huduma nyingine	6,768,927	8,892,747	10,628,874	10,551,937	12,285,162	49,127,647	84%
Gharama za Uendeshaji FCS	1,615,300	1,914,800	1,799,490	1,889,164	1,995,923	9,214,677	16%
Jumla	8,384,227	10,807,547	12,428,364	12,441,101	14,281,085	58,342,324	100%

9. Mtazamo wetu kuelekea Maendeleo:



Timu ya Uhariri

ADAM LINGSON

PHILIP CONNELY

ELIZAPH J. DEO

BERNARD KINDOLI

NEEMA YOBU

ISRAEL LAIZER

ZAA TWALANGATI

EVARISTO HAULLE

KIMEANDALIWA NA HAKIKAZI CATALYST

THE FOUNDATION
for Civil Society

The Foundation for Civil Society
Haidery Plaza, Ghorofa ya 5, Mtaa wa Upanga/Kisutu
S.L.P 7192, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2138530/1/2
Nukushi: +255 22 2138533
Barua pepe: information@thefoundation-tz.org
Tovuti: www.thefoundation-tz.org